**MAELEZO YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA KUKABIDHI HUNDI KWA AJILI YA HEWA UKAA, WILAYA YA TANGANYIKA, MKOA WA KATAVI**
**TAREHE 23 JULAI, 2022**

- **Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo,**
- **Mheshimiwa Mwanamvua Mrindoko, Mkuu wa Mkoa wa Katavi**
- **Mheshimiwa Beda Katani, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Katavi,**
- **Mheshimiwa Rodrick Mpogolo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi,**
- **Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Katavi,**
- **Viongozi wa Chama na Serikali mliopo,**
- **Viongozi wa vyama vya siasa mliopo,**
- **Ndugu Viongozi wa Dini,**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Ndugu Wananchi, Wageni Waalikwa wote, Mabibi na Mabwana.**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania….**

Napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupatia afya njema, kutusafirisha salama na kutuwezesha kufika hapa Katuma, Wilaya ya Tanganyika. Leo ni siku yangu ya tatu hapa Mkoa wa Katavi na nimekuja kuwasalimu lakini pia kukagua shughuli za maendeleo. Nawashukuru sana wananchi kwa mapokezi mazuri tangu nifike. **Asanteni sana!**

Napenda kutumia fursa hii kuwasilisha salaam za upendo kutoka kwa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais anawasalimia sana na anawaomba muendelee kuchapa kazi. Vilevile, napenda kuwapongeza sana Wananchi wa Mkoa huu kwa kuwa wachapa kazi kwelikweli. Katavi ni moja ya Mikoa hapa nchini ambayo inategemewa sana kwa

uzalishaji wa mazao ya chakula na kulisha mikoa mingine na nje ya nchi. **Hongereni sana!**

***Ndugu Viongozi, Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Kama nilivyotangulia kusema nimekuja kukagua utekelezaji wa shughuli za maendeleo lakini pamoja na hilo, leo nimekuja hapa Wilaya ya Tanganyika kuwakabidhi mfano wa hundi ya fedha iliyopatikana kwa mauzo ya Hewa Ukaa. Sina hakika kama watanzania wengi wanafahamu nini maana ya hewa ukaa au nini kilichofanyika hadi kupatikana kwa fedha hizi.

Ningependa nitumie muda huu mchache kuwaeleza kwa ufupi sana nini maana ya tukio hili la leo.

Hewa ya ukaa kwa urahisi kabisa ni hewa tunayoitoa tukipumua. Sasa hewa hii pamoja na gesi joto nyingine, ikiwa nyingi sana hewani kupita kile kiasi kinachotakiwa kisayansi, inasababisha madhara kama mabadiliko ya hali ya hewa ambayo ndio tunaita mabadiliko ya tabia nchini. Na sote ni mashahidi kuwa, mabadiliko ya tabia nchi yamesababisha athari kubwa hususan mabadiliko ya mvua na majira ambayo yanaleta athari kwenye kilimo; na pia athari nyingine ni kuyeyuka kwa barafu na theluji katika milima yetu ambayo pia inaleta athari kwenye kina cha bahari. Nimechagua hizi athari chache ambazo tunaweza kuzielewa kirahisi. Sote tuelewe kwamba Tanzania kama nchi nyingine duniani, inakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi, kupotea kwa uoto wa asili na uchafuzi wa mazingira. Hivyo, katika kukabiliana na kudhibiti mabadiliko ya Tabianchi, nchi zinazoendelea kama Tanzania, zinahimizwa kupanda miti kwa wingi ikiwa ni pamoja na kuhifadhi misitu. Uhifadhi wa misitu unasaidia kupunguza hewa Ukaa na kuongeza upatikanaji wa hewa safi. Kwa mantiki hiyo, ili kuhamasisha nchi kupanda miti na kuhifadhi misitu, kuna mikataba ya kimataifa ambayo inahamasisha biashara ya hewa ukaa duniani. Hii ina maana kwamba, tunapopanda miti na kuhifadhi misitu ambayo inasaidia kufyonza na kupunguza hewa ukaa hewani, tunalipwa!

Na hii ndio sababu, wananchi wa Wilaya ya Tanganyika, leo mnapokea hundi ya fedha kiasi cha **TZS 2,300,000,000/=** iliyopatikana kwa mauzo ya Hewa Ukaa! Nawapongeza sana kwa jitihada zenu za kuhifadhi mazingira na kupitia uhifadhi huo kunufaika na biashara ya Hewa Ukaa. **Hongereni sana!**

***Ndugu Viongozi, Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Kama ilivyoelezwa mradi huu wa Hewa ya Ukaa ulianza mwaka 2018 ukiendeshwa na Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, kupitia Taasisi ya CARBON TANZANIA kwa kushirikiana na taasisi ya TUUNGANE. Na kwamba kupitia mradi huu, zaidi ya wakazi 34,242 kutoka vijiji nane (8) vya Lugonesi,

Mwese, Lwega, Bujombe, Kapanga, Katuma, Mpembe na Kagunga ndani ya Tarafa ya Mwese wanafaidika na mradi huu. **Hongereni sana!**

Nimepewa taarifa hapa kwamba Halmashauri kupitia misitu ya Tongwe Mashariki na Tongwe Magharibi yenye jumla ya ukubwa wa Hekta zaidi ya 500,000, imeingia makubaliano na Taasisi ya CARBON TANZANIA kwa ajili ya kuingia katika mpango huo. Nafurahishwa na mwamko huu. Ni matarajio yangu nitasikia Halmashauri nyingi zaidi nchini zikihamasika pia.

***Ndugu Viongozi, Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Biashara ya hewa ya ukaa inalipa! Wilaya ya Tanganyika mmekuwa mashahidi, kwani mmejionea fedha zinazopatikana kwenye biashara hii ya hewa ya ukaa zimepelekwa kwenye vijiji vya mradi na pia Halmashauri yetu ya Wilaya imekuwa ikinufaika kwa kupata asilimia 10 ya faida.

Kupitia mradi huu, mtaweza kuboresha huduma kwa jamii pamoja na kuhusisha jamii katika uhifadhi na unufaikaji wa moja kwa moja na faida za uhifadhi. Aidha, mradi huu utawawezesha wananchi kufanya shughuli za maendeleo za vijiji kupitia mapato yatokanayo na kuuza Hewa Ukaa baada ya kuhifadhi Misitu yao kwa kuzuia uharibifu au ukataji miti katika maeneo ya vijiji yaliyohifadhiwa na kusimamiwa kisheria na wanajamii wenyewe.

***Ndugu Viongozi, Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Kumekuwa na ongezeko la biashara ya Hewa Ukaa duniani. Kuna aina mbili za masoko ya Hewa Ukaa ambazo ni Soko Huria na Soko la Umoja wa Mataifa. Kwa sasa, mataifa yaliyojikita katika biashara hii, yanatumia Soko Huria, kutokana na ugumu wa mikataba inayoendana na Soko la Kimataifa. Aidha, kupitia Soko Huria, kumekuwa na makampuni binafsi ambayo yamejikita katika biashara hii ya Hewa Ukaa.

Nitumie fursa hii kumuelekeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya kutosha kuhusu fursa zilizopo katika biashara ya Hewa Ukaa. Aidha, Mheshimiwa Waziri ahakikishe mapungufu yote ya kisera na usimamizi wa biashara ya Hewa Ukaa yanapatiwa ufumbuzi na Taifa letu kunufaika na biashara hii. Kwa upande wa Wananchi napenda kusisitiza yafuatayo:

> **Kwanza,** nawaomba muendelee kutunza mazingira ili muendele kunufaika na biashara hii ya hewa ukaa. Nafahamu wapo baadhi ya wananchi wanaokata miti na kuchoma moto hovyo kwa ajili ya maandalizi ya mashamba na mikaa. Ninawaomba wananchi wenzangu acheni kabisa tabia hiyo. Uongozi wa Mkoa chukueni hatua kali za kisheria kwa yeyote

mtakaembaini amevunja utaratibu tuliojiwekea. Jamani tutunze mazingira ili nayo yatutunze.

**Pili,** nimeelezwa hapa kuwa mmeweza kupata mazao pamoja na ziada. Hata hivyo kama wengi mnavyofahamu mwaka huu sehemu nyingi hazijapata mvua za kutosha na meneo mengi ya nchi yetu hawajapata mazao ya chakula ya kutosha. Ninyi hapa mmebahatika mmevuna na mmepata ziada. Ninawaomba tumieni mazao hayo lakini mkumbuke kuweka akiba. Msiuze mazao yote hadi mkakosa akiba.

**Tatu,** nimestushwa na takwimu kwamba Mkoa wa Katavi ni kati ya mikoa yenye Watoto wenye tatizo la utapiamlo kutokana na kukosa lishe bora. Hili limenishangaza sana kwa kuwa mkoa huu umejaliwa kuwa na kila aina ya mazao. Jamani kwa mikoa yenye chakula cha kutosha jambo hili hapana! Ninawaelekeza Viongozi wa Mkoa kwa kushirikina na Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wote wa Halmashauri mtoe elimu kuhusu umuhimu wa lishe bora kwa Watoto tangu wakiwa tumboni kwa mama zao. Mtoto akikosa lishe bora hata darasani anakuwa na uwezo mdogo sana.

**Nne,** ni tabia ya Wazazi kuruhusu ndoa za utotoni na wanaume kuwapa mimba Watoto wa shule hali inayosababisha Watoto hao kusitisha masomo. Hili ndugu zangu nasema tena hapana! Acheni kabisa tabia hii. Wapeni nafasi Watoto wa kike wasome na wamalize shule. Hatua kali za kisheria zitachuliwa kwa Mzazi yeyote atakaebainika kumuozesha mtoto wakati hajamaliza shule.

***Ndugu Viongozi, Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Kabla sijamaliza hotuba yangu, napenda nitumie fursa hii pia kutoa maelekezo yafuatayo kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira:

**Kwanza**, Simamieni Sera na Sheria ya mazingira ili kupunguza na hatimaye kuondoa uharibifu na uchafuzi wa mazingira;

**Pili**, fanyeni tathmini za athari za kimazingira, ukaguzi wa kimazingira na ufuatiliaji wa kimazingira katika maeneo mbalimbali ya mkoa huu na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sera na Sheria zetu za Mazingira;

**Na mwisho**, toeni elimu na kukuza mwamko wa jamii juu ya umuhimu wa utunzaji na usimamizi bora wa mazingira pamoja na ushiriki wa jamii katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwenye maeneo yao; na

hususan jinsi ambavyo jamii zinaweza kufaidika na mauzo ya Hewa Ukaa.

***Ndugu Viongozi, Wananchi, Mabibi na Mabwana;***
Naomba nihitimishe hotuba yangu kwa kuwakumbusha kuwa, nchi yetu itafanya Sensa ya Watu na Makazi tarehe 23, Agosti 2022. Nawaomba wananchi wote wajitokeze kuhesabiwa na kutoa kila aina ya ushirikiano utakaohitajika kufanikisha zoezi hili muhimu kwa mipango ya maendeleo ya Taifa letu.

***Mwisho kabisa***, niwashukuru wote kwa kufika kwenye shughuli hii muhimu ya kukabidhiwa Hundi kwa kuwekeza katika uhifadhi wa misitu.

**Mwenyezi Mungu Awabariki sana.**

**Asanteni kwa kunisikiliza!**